# KUDUMU KATIKA KAZI YA BWANA

Maisha ya Kikristo ni maisha yaliyojaa kazi ya Bwana (1Wakorintho 3:9). Twaimba nyimbo za kazi, bali kwa kweli, ni wachache wadumuo katika kazi ya Bwana. Twaimba, "Nataka kuwa mtenda kazi kwa ajili ya Bwana", hivi lakini, kweli tunamaanisha? Kusema kitu ni jambo moja, na kutekeleza kilichosemwa ni jambo jingine kabisa. Kazi ya Bwana hujumisha manufaa, majukumu na tunu kubwa zaidi ya kazi yoyote aliyopata kuijua mwanadamu. Katika makala hii, tunataka kutafakari maana ya kudumu katika kazi ya Bwana kama ilivyoelezwa na Mtume Paulo katika 1 Wakorintho 15:58

## UPANA WA KAZI

Himizo la Paulo liliwalenga "ndugu zangu wapendwa". Halikuwalenga  wazee wa kanisa peke yao, ingawae wanatakiwa kuwa vielelezo (1 Petro 5:3). Halikuwalenga mashemansi peke yao, ingawaje neno shemansi maana yake ni "mhudumu" (Matendo 6:1-3). Halikuwalenga wahubiri peke yao, hata ingawaje wana kazi ya kufanya (2Timotheo 2:15; 4:5)

Agano Jipya linafundisha ya kuwa kila mkristo lazima awe mtenda kazi. Mfano wa talanta katika Mathayo 25:14-30 huthibisha wazi wazi jambo hili. Hata kama wote tutakuwa na talanta moja tuna kazi ya kufanya. Kanisa la Agano la Jipya linaonyeshwa kuwa mwili ( Warumi 1:22,23). Kama ilivyo kwa upande wa mwili wa nje, kila kiungo katika mwili wa kiroho wa Kristo kina utendaji unaotakiwa kutekelezwa (1 Wakorintho 12:12-21). Kwa kulitazama hili, kutakuwa na utofauti wa kiutendaji lakini bila kukosekana. Kutakuwa na tofauti wa vipaji, shauku, fursa, na kuendelea, hakutakuwa na tofauti kwa misingi ya elimu, umri, jinsia, n.k. (Matendo 8:4). Katika kanisa daima kutakuwa na kazi kwa ajili ya Paulo na Timotheo; kwa ajili ya Eunke na Dorkasi; na kwa ajili ya Barnaba na Marko. Kwa maneno mengine, daima kazi itakuwepo kwa ajili ya kila mtu.

## VIGEZO VYA MSINGI VYA KAZI

Ushawishi wa ndani unaojumuisha uimara, kutoyumba, ni vya lazima kwa kazi ya Bwana. Mashaka na maoni viliwazuia Wakorintho katika kazi yao;

**Tatizo la kula nyama iliyotolewa kama kafara kwa sanamu-Sura ya 8**
**Maswali juu ya kilemba na meza ya Bwana- sura ya 11**
**Umuhimu wa kutumia karama za rohoni**

Wafilipi walishauriwa kuwa imara na kusimama katika roho moja wakishindania imani ya injili (Wafilipi 1:27). Bidii katika Bwana haiwezekani bila kuwapo imani na ushawishi thabiti wa ndani (Yakobo 2:18). Kazi yetu ina uwiano na imani yetu, ushawishi wa ndani na tumani letu.

## UENDELEVU WA KAZI YA BWANA

Dini ya Kristo ni dini ya "siku zote"

**Maneno yenu yawe na neema siku zote,-Wakolosai 4:6**
**Furahini katika Bwana siku zote- - Wafilipi 4:4**
**Tii siku zote - Wafilipi 2:12**
**Mwe tayari siku zote kujibu - 1 Petro 3:15**

Kufanya kazi maana yake ni “kuwa tayari wakati ukufaao na wakati usiokufaa” – 2Timotheo 4:2

Utumishi wa msimu haukubaliki kwa Mungu. “Siku zote” humaanisha siku sita kwa juma ongeza jumapili. Utumishi wa jumapili tu siyo utumishi mwema. “Siku zote” humaanisha wakati tunapotazamwa na kusifiwa ongeza tunapokuwa hatuonwi na bila kusifiwa. “Siku zote” humaanisha wakati wa matukio maalum kama mikutano ya injili, VBS, n.k., pamoja na majuma mengine katika mwaka. “Siku zote” humaanisha tuwapo vijana na tunapokuwa siyo vijana (Luka 9:62)

Kukosekana kwa uendelevu katika utumishi wa kikiristo humaanisha kuwa sisi sio wa kutegemewa. Yawezekana tukawa “moto”, au pengine “baridi”, au labda tu “vuguvugu”. Pia yaweza kumaanisha kuwa tunachukua nafasi katika wokovu wetu wa milele.

## MGUSO WA KAZI YA BWANA

Neno la Kiyunani ambalo kwalo limetafsiriwa neno “kudumu” linavutia unapojifunza. Ni neno “perisseuo” na humaanisha “kuwa juu; zidi. “ Limetumika katika kuzidi mengine katika Mathayo 5:20. Limetumika ili kuzidisha kiwango katika aya kama vile Luka 15:17. Limetumika kuzidisha lililotendeka zamani, jambo kama hilo linaonekana katika Marko 15:14.

Utumishi wa kikristo lazima uwe endelevu katika kudumu. Utumishi wa kudumu ni utumishi wa hiari. “Walioajiriwa alfajiri” hufafanua jambo hili kama lilivyo katika Mathayo 20:1-20. Utumishi wa kudumu ni utumishi wenye bidii kama inavyoelezwa na Mtume Paulo katika Warumi 12:11. Utumishi wa kudumu unatoka moyoni (Waefeso 6:6), na utumishi unatangulizwa (Mathayo 6:33).

## NIA YA KAZI YA BWANA

Ufufuo wa mwisho unatumika kama msukumo kwetu kufanya kazi ambayo ametupa Mungu tuifanye. Neno “Kwa hiyo” katika 1 Wakorintho 15:58 linaiunganisha na mistari iliyotangulia. Sura nzima inazungumzia ufufuo na kuvaa mwili usio kufa. Anachosisitiza Paulo hapo ni kwamba, kwa kutazama ukweli kwamba kuna uhai baada ya huu, Wakristo wanatakiwa kufanya kazi. Jambo hilo hilo lilisemwa na Yohana katika ufunuo 14:13. Uhai baada ya kaburi ni sababu yetu sote kudumu katika kazi ya Bwana.

Hukumu ya mwisho hutumika kama msukumo. Neno “kwa kadri” huashiria siku ya kuhesabu. Siku ya hukumu itakuwa ni siku ya wanadamu wote kutoa hesabu (Warumi 14:12: 2 Wakorintho 5:10. Itakuwa ndiyo siku ya ijara kulingana na jitihada zinazofanyika wakati wa uhai huu.

(Wagalatia 6:9). Kazi yetu mara nyingi inaonekana kuwa ni bure wakati huu, kwa Bwana taabu yetu si bure. Uhakika wa Neno ni uhakika wa ijara ya taabu zetu katika Kristo.

ASILI YA KAZI – Ingawaje halijajumuishwa katika 1 Wakorintho 15:58, kazi ya Bwana ni ile ambayo alituamuru kuifanya,  na impayo utukufu, na impayo heshima anayostahili.

Kufanya kazi kwa ajili ya Bwana humaanisha kufanya mapenzi ya Mungu. - Yohana4:34
Kufanya kazi kwa ajili ya Bwana humaanisha kumheshimu Wafilipi 1:20

Kazi ya Bwana ni kazi inayojumuisha mambo yafuatayo;

Uinjilisti – Kumtangaza Kristo na wokovu wake kwa watu wengine (Marko 16:16; Warumi 1:16)
Matendo mema- hili hujumuisha kuwagawia ulivyo navyo wasio na kitu (Wagalatia 6:10)
Kujengana – Hili huhusiana na kujengana sisi kwa sisi kwa kujifunza, Ibada, n.k. (Waefeso 4:12)

Kudumu katika kazi ya Bwana humaanisha furaha hapa na baadaye mbinguni. Tunatakiwa kuukagua utumishi wetu na kujiuliza “Hivi, ninadumu katika kazi ya Bwana?” Hivi ni muhimu kukumbuka kwamba swali siyo “Hivi, ninafanya kazi ya Bwana muda muda?” bali ni “Hivi, ninadumu katika hiyo kazi?” .Tukumbuke, “usiku waja, mtu asipoweza kufanya kazi” (Yohana 9:4)